**Deutsche Welle**
**"Learning By Ear"**
**MAFUNZIO NA KAZI : SEKTA YA JUA KALI**

**Mwandishi : Richard Lough, Kenya**
**Wahariri : Ulrich Neumann, Maja Dreyer**
**Tafsiri: Eric Ponda**

**1 Msilimuzi/**
**Kufunga na kufungua**
**3 Sauti : Peter, Mvulana muuzaji Mtunda, Mama**

**Scholastica- Mchuuzi barabarani,Julius-mchuuzi vitoto vya mbwa barabarani**

**Intro**

Hujambo na karibu kwa makala mengine ya "Learning by Ear". Makala yanayozungumzia masuala ya mafunzo na Kazi, tunapokukutanosha na watu wa taaluma mbali mbali . Hivi leo tunatembelea vitongoji vya mji wa Nairobi na kukutana na wafanyi kazi katika sekta isiyo ya kirasmi. Katika eneo hili, tunakutana na wafanyi kazi wengi wao huwakusoma sana , na kusalia tu kufanya kazi ngumu , huku pato lao likitegemea zaidi biashara ndogo ndogo. Andamana nasi….

**1. SFX Atmo Straße**

Mtaa wa Kilimani ni kitongoji kilichoko kilomita chache tu kutoka kati kati mwa Jiji la Naiorobi. Ni mtaa wenye mazingiza mazuri na miti mingi,ukikaliwa hasa wengi wa watu wenye pato la kadri nchini Kenya na vile vile kupendwa sana sana nawageni waofanya kazi Jijini. Tuko katika barabara ya Argwings Khodek, Barabara kuu inayounganisha kitogoji hicho na kati kati mwa jiji la Nairobi. Mara nyingi hasa wakati wa mchana, barabara hii huwa na shughuli nyingi na msongamano wa magari. Hii ndio sababu umepelekea kupendwa sana na na wafanyi kazi wa sekta hii isiyo rasmi inayofahamika sana nchini Kenya kama "Sekta ya Jua Kali",yaani watu wanaofanya kazi siku nzima chini ya

mazingira ya Jua kali. Kwa hivyo andamana nasi tunapokutana na kuzungumza na baadhi yao kuhusu kazi wanazozifanya …..

**2. SFX Makalele ya barabarani**

**3. O-Ton: Muazaji matunda 1**

Jina langu ni Peter Muamaingay. Niko hapa kituo cha biashara cha Yaya Centre, kuuza mboga na matunda.

Kibanda chake kimepangwa bidhaa nyingi tu za mboga na matunda, Yako mananasi, Nyanya, ndizi, vitunguu na Saladi vikiwa vimepangwa kwenye vijisanduku vya mbao. Ni saa tano asubuhi hivi, na tayari Peter amefanya kazi kwa zaidi ya masaa tano tangu afungue biashara yake asubuhi na mapema.

**4. O-Ton: Muuzaji wa 2**

Mimi huamka asubuhi na mepema na kufukia mwendo wa saa 12, alfajiri tayari huwa nimefika hapa. Ninapofika huanza kupanga kazi yangu, mboga, matunda na kadhalika na kuanza kuwauzia wateja ambao huwasili mapema. Huendelea kuuza hadi saa moja usiku.

Peter anasema kuwa faida anayopata ni kidogo mno ikilinganishwa na masaa anayofanya kazi. Kwa mfano hununua kilo moja ya Tomato kwa shilingi 30, chini ya nusu ya Dola na kisha kuuza kwa shilingi 50 na kupata faida kidoko tu. Peter anasema kuwa biashara hiyo huwa nzuri wakati wa mwanzo mwanzo mwanzo wa mwezi wakati watu wanapokuwa wamepokea mishahara yao. Peter amefanya kazi hii kwa zaidi ya miaka 10 na najihisi muuzaji hodari. Je siri yake ni nini?

**5. O-Ton: Muuzaji Matunda 3**

Ukitaka kuwa muuzaji au mfanyabiashara mzuri lazima uwe mtu asiyekuwa na hasira.. Hilo ni muhimu! Kwa sababu utakutana na watu tofauti na baadhi yao watasema hawataki bidhaa zako. Hivyo basi lazima uwe mnyenyekevu na kuwashawishi ili kuvunja makali ya hasira zao ndiposa mutaweza kuzungumza na kuelewana. Ukiwa mtu wa hasira, basi wateja wako watakasirika zaidi na hapo biashara yako itaathirika.

Eneo la barabara anakofanyia biashara Peter na wengine halina maduka. Wachuuzi katika barabara hii wamejenga vibanda tu kuuzia bidhaa zao. Na wengine hawana hata hivyo vibanda .
Upande mwengine wa barabara, yupo mama anayeuza nguo kuu kuu. Wako wachuuzi wengi tu kando kando ya barabara hii wanaouza nguo kuu kuu ikiwa ni pmaoja na mavazi ya kuogelea kwa wanaume na wanawake.Pia kuna kofia zinlizotengenezwa kwa majani zikining´inia pembeni mwa vibanda hivyo…..

**6. O-Ton: Mchuuzi wa 1**

Naitwa Scholastika Njoki. Natoka kabila la Wakikuyu na ni mama wa watoto watatu. Ni na biashara yangu upande ule mwingine wa barabara….

Kila asubuhi Scholastika, huanza shughuli zake mwendo wa saa mbili na nusua asubuhi. Anasema si rahisi kufanya biashara kando kando mwa barabara. Kwani wakati wa Jua kali huwa ni shida na ikinyesaha pia shughuli zao hukwama kabisa

**7. SFX Mchuuzi wa mavazi ya Kuogelea.**

Scholastica sasa anazungumza na mteja wake wa pili tangu afungue biashara asubuhi hii. Lakini anasema kuwa mara nyingi biashara huwa mbaya na vigumu kuuza, lakini wakati mwengine biashara inapokuwa nzuri Scholastika anaweza kupata shilingi 500 kwa siku, karibu dola saba hivi,…ambazo anasema hazimtoshi.

**7. O-Ton: Mchuuzi wa 2**

Mimi siwezi kuweka akiba ya hadi shilingi 500 kwa siku, na nikiweza kufanya hivyo itakuwa ni bahati tu. Pesa hizi zina matumizi mengi, kununua sabuni, unga na vitu vingine vidogo vidogo. Kwa kweli siwezi kuweka akiba kutokana na biashara hii.

Kwa sababu sehemu wanazofanyia biashara ni maeneo ya mabanda, wengi wa wafanyi biashara hao hawalipi kodi. Na hii ndio sababu mara nyingi utakuta wakizozana na maafisa wa baraza la jiji la Nairobi,ambao hutokezea mara kwa mara wakitafuta hongo au kuwafukuza na kuwachukulia mali zao…

**8. O-Ton: Mchuuzi wa 3**

Mara nyingi huja na kutuitisha ada ya shilingi 25 na hata mara nyingine wanataka hongo. Lakini wanapokuwa wengi huitisha hongo ya hadi shilingi 300 au shilingi 500, na ukikosa kuwapa hongo wanachukua mali yako.

Scholastica anasema kuwa maafisa hao wa baraza la jiji baadaye huenda kuuza mali hiyo kwa manufaa yao wenyewe.Wakati mwengine huwarejeshea wachuuzi mali zao, lakini kwa ada ya juu.

**9. O-Ton: Mchuuzi wa 4**

Huitisha pesa nyingi sana. Unapokamatwa na maafisa wa baraza, unatozwa faini ya hadi shilingi elfu 5. Na ukiangalia biashara yenyewe

mtu huwezi kupata shilingi elfu 5, lakini unatozwa zaidi ya kiwango hicho. Kwa hivyo badala ya kwenda kulipa faini hiyo ya shilingi elfu 5, mimi huona kheri kuwaachia kisha niende kutafuta pesa kidogo kutoka kwa jirani na kuwahonga ili wanirudishie mali yangu.

**10. fade into SFX_ Mazingira ya Sarit**

Mbali na hayo kunavitongoji vingine au mitaa yenye vituo bora zaidi vya kibiashara kuliko mtaa huu wa Kilimani. Kwa Mfano mtaa wa Westlands ambako utapata maduka makubwa ya Sarit Centre. Maduka haya hutembelewa sana na Wakenya matajiri au raia wa kigeni wanaoishi mitaa ya kifahani Jijini.Lakini mbali na hayo, utakumbana na wachuuzi wametapakaa kila mahali wakiuza bidhaa zao kati kati mwa jiji, bidhaa kama vile kuanzia DVD, viatu , nguo kuukuu na hata watoto wa Mbwa.

**11. O-Ton: Muuzaji wa kwanza wa Vitoto vya Mbwa**

Mimi ni Julius Kinyanjui. Ni na umri wa miaka 29. Hufanya biashara hii ya kuuza watoto wa mbwa. Kwa kawaida huwauzia Wakenya wanaotaka kuimarisha usalama wa majumbani mwao au hata kwa kampuni zinazotoa huduma za usalama.

**12. SFX_VITOTO VYA MBWA:**

Julius mwenye umri wa miaka 29 pamoja na wenzake, wanaonekana wakitembea barabarani hasa karibu na mizunguko ya barabara wakibeba vitoto hivyo vya Mbwa huku wakijaribu kuwauzia wenye magari. Julius hununua vitoto hivi kutoka kwa wafugaji wa Mbwa. Na mara nyingi hutegemea aina ya Mbwa. Lakini wale ghali zaidi ni aina ya Rottweilers ama Dobermans wanaopendwa sana na walinzi. Kwa

mfano kitoto cha Mbwa aina ya Rottweiller kinaweza kugharimu dola 20 …

| **13. O-Ton: Muuzaji wa pili wa Vitoto vya Mbwa** |
| --- |
| Naweza kupata kwa shilingi 1500 na kuuza kwa shilingi 2000 au 2200. Kwa takriban wiki moja naweza kuuza vitoto vine au vitano. Mara nyingine unaweza kukaa siku mbili au tatu bila ya kuuza chochote. |

Julius ni miongoni mwa Wakenya wengi tu wanofanya kazi katika sekta ya Jua Kali. Yeye hana kisomo na vyeti vinavyomwezesha kutafuta kazi. Na kwa hivýo ni vigumu kupata kazi. Lakini yeye anafurahia kufanya kazi hii inayompa pato la kila siku badala ya kukaa ovyo bila chochote cha kufanya. …

| **14. O-Ton: Muuzaji wa 3 Vitoto vya Mbwa-** |
| --- |
| Mimi hufanya kazi kwa sababu sina kazi nyingine ninayoweza kufanya. Kutokana na umaskini hapa nchini Kenya, ni lazima mtu afanye bidii ili apate kitu cha kula. Kwa wiki moja naweza kupata shilingi 1,500. Ni afadhali kwa sababu kazi hii inanipa chakula cha kila siku.. |

Tunaachana na Julius ili aweze kuendelea na kazi yake. Julius anaungana na wachuuzi wengine waliotapakaa kila mahali wakiuza bidhaa zao katika barabara za jiji la Nairobi.

**Sauti ya Mazingira ya jiji ikitoweka.**

**Outro**

Barani Africa , wengi wa wachuuzi wa barabarani wanakabiliwa na hali ngumu ya maisha . Hulazimika kufanya kazi kwa masaa mengi zaidi ili

kukidhi maisha yao. Mtu anapokuwa bila elimu ya kutosha , hujikuta katika sekta hii ya Jua kali. Ukitaka kujua mengi zaidi kuhusu mafunzo na kazi za aina mbali mbali , au iwapo unataka kukisikiliza tena kipindi hiki, unaweza kutembelea mtandao wetu www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwa makala mengine ya "Learning by Ear" kuhusu mafunzo na kazi, ungana nasi kwa kipindi kijacho. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.